JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA PILI

Februari 2024



## Tumuenzi hayati Lowassa kwa vitendo – Rais Samia

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA.

www.pmo.go.tz



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Watanzania tuna wajibu wa kuendelea kustahimiliana na kufanya siasa za kistaarabu zinazoweka mbele maslahi ya nchi.

Rais Samia amesema hayo wakati wa ibada ya mazishi ya aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu, Hayati Edward Ngoyai Lowassa yaliyofanyika katika kijiji cha Ngarash wilayani Monduli.

Aidha, Rais Samia amesema njia pekee ya kumuenzi Hayati Lowassa ni kuendesha siasa kwa kuheshimiana, kustahamiliana ili kuleta maendeleo bila kutikisa misingi ya utaifa na mshikamano wetu licha ya kutofautiana mitazamo, misimamo na sera.

Vile vile, Rais Samia amesema Hayati Lowassa alikuwa muumini wa elimu kama nyenzo ya kujikomboa na umasikini, hivyo alipenda vijana wapate maarifa na ujuzi kwa ajili ya ustawi wa familia zao na jamii kwa ujumla.

Rais Samia pia amesema katika sekta ya elimu, Hayati Lowassa alisimamia kwa mafanikio Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) akiwa Waziri Mkuu kwa kuratibu na kusimamia ujenzi wa shule za Sekondari katika kila Kata nchini.

Hali kadhalika, Rais Samia amesema tangu wakati huo serikali imeendelea kusimamia ujenzi na uendelezaji wa shule za Kata kote nchini, na hivyo kuongeza shule za Serikali kutoka 828 mwaka 2004 hadi shule 4,578 mwaka 2023.

Kwa kutambua umuhimu wa elimu yenye kukidhi mahitaji ya soko la ajira mwaka 2023 serikali imefanya mabadiliko ya Sera na Mitaala ya Elimu ili kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi mahitaji ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia.




Kwa upande mwingine, Rais Samia amesema Taifa limepoteza moja ya viongozi mahiri, mpenda maendeleo, mwanamageuzi na kipenzi cha wengi.



Uwekezaji mkubwa wa Serikali wafanikisha ukamataji wa shehena ya dawa za kulevya

Serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imesema imepata mafanikio makubwa katika mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya ambapo kuanzia mwezi Januari hadi Disemba 2023 kilogramu zaidi ya milioni moja za aina mbalimbali za dawa za kulevya zilikamatwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama wakati akizungumza na waandishi wa habari Jijini Dodoma kuhusu taarifa ya mafanikio ya Serikali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya .




Mhe. Jenista alisema Watuhumiwa 10,522 walikamatwa ambao kati yao wanaume ni 9,701 na wanawake ni 821 huku akisema kuwa jumla ya hekari 2,924 za mashamba ya bangi na mirungi ziliteketezwa.

"Kiasi cha dawa zilizokamatwa kwa mwaka mmoja ni zaidi ya mara tatu ya dawa za kulevya zilizokamatwa kwa kipindi cha miaka 11 hapa nchini, kwani miaka 11 iliyopita tulifanikiwa kukamata kilogramu 660,465 pekee. Aidha, Serikali imefanikiwa kuzuia uingizaji wa kilogramu 157,738.55 za kemikali bashirifu ambazo zingeweza kutumika kutengenezea dawa za kulevya kinyume cha sheria," Alisema Mhe. Jenista.

Waziri Jenista amesema mafanikio ya ukamataji huu yanatokana na nia, utashi na dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan.

"Mara baada ya kuingia madarakani ameonesha dhamira yake kwa vitendo katika kuiimarisha Mamlaka kwa kuipa vitendea kazi vinavyohusianisha teknolojia ya kisasa ya kimkakati katika mapambano, kutoa mafunzo kwa watumishi ndani na nje ya nchi pamoja na uzalendo wa watendaji

kwenye Mamlaka,"Alieleza

Pia aliongeza kwamba Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imesaini hati ya makubaliano ya ushirikiano (MoU) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa lengo la kutoa elimu ya dawa za kulevya na rushwa kupitia klabu za kupinga rushwa nchini ambapo sasa zitaitwa klabu za kupinga rushwa na dawa za kulevya.

"Tafiti zinaonesha kwamba, matumizi ya dawa yanaanza katika umri mdogo kati ya miaka 10 na 12 hivyo Serikali imeona iweke mkazo huko kwani watoto wengi wanapitia katika shule hizo na elimu imeendelea kutolewa katika makundi ya kijamii yakiwemo ya viongozi wa dini, viongozi wa kimila, waandishi wa habari, vyombo vya ulinzi na usalama,



"Ujenzi wa nyumba za waathirika wa maafa Hanang' uzingatie ubora na thamani ya fedha," Waziri Mhagama

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera Bunge na Uratibu Mheshimiwa Jenista Mhagama amehimiza ujenzi wa nyumba za waathirika wa maafa ya maporomoko ya tope, miti na mawe Wilayani Hanang' Mkoa wa Manyara uzingatie viwango na thamani ya fedha ili kuhakikisha hatua ya kurejesha hali kwa wananchi hao inakuwa yenye viwango na ubora unaotakiwa.

Ametoa kauli hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari tarehe 10 Februari, 2024 mara baada ya kuhitimisha ziara yake ya kikazi ya kukagua na kujionea maendeleo ya hatua za kurejesha hali katika maeneo mbalimbali Wilayani humo yalipotokea maafa hayo Disemba 3, 2023 na kusababisha vifo, uharibifu wa mali pamoja na miundombinu ikiwemo barabara.

Waziri Mhagama amesema, Serikali imeona umuhimu wa kujenga nyumba 108 zitakazotumika na waathirika wa maafa hayo ambapo eneo lililotengwa ni Gidagamowd lililopo katika Kitongoji cha Waret ambalo lina ukubwa wa Hekari 100 na tayari viwanja 269 vimepimwa.

"Mhe Rais wetu amejali sana, na ameonesha moyo kama mama kuamua kutenga eneo hili maalum na kutoa maelekezo ya kuhakikisha wale wote waliopata changamoto hii wanapata makazi mapya, hivyo ni muhimu kutimiza maagizo haya kwa viwango vya juu na ubora unaotakiwa," alieleza

Aidha amesema kuwa, ujenzi huo uende sambamba na ujenzi wa shule, vituo vya afya na kituo cha polisi ili wananchi wapate huduma za kijamii kwa wakati na urahisi wawapo hapo.

Amezitaka Taasisi zote zinazopaswa kuhakikisha huduma muhimu zinaanza kupatikana ikiwemo; umeme, maji na barabara zikamilike kwa wakati bila kukwamisha zoezi la ujenzi wa nyumba hizo.

"Ni lazima taasisi zetu ikiwemo TANESCO na TARURA mjitahidi kurahisisha upatikanaji wa huduma zenu hasa ya kuchonga barabara hii ili kuwe na urahisi wa mawasiliano na kuhakikisha wakandarasi hawakwami na kazi ya ujenzi inaanza mwezi huu wa Februari na tunataraji ukamilike mapema Mei, 2024," alisisitiza Waziri Mhagama

Alitumia nafasi hiyo kuwashukuru wadau walioendelea kutoa misaada ya kibinadamu kwa waathirika hao huku akiwaomba wengine kuendelea kufanya hivyo ili hatua hiyo ya kurejesha hali ikamilike na wananchi warejee na maisha yao kama awali.

Naye Mkuu wa Wilaya hiyo, Mheshimiwa Janeth Mayanja amemshukuru Mheshimiwa Waziri Mhagama kwa kuendelea kuratibu kila hatua ya masuala ya menejimenti ya maafa huku akiahidi kuendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha adhma ya kukamilisha ujenzi huo inafikiwa.



""Bodi isaidieni NEEC katika kufanikisha azma ya serikali"
Naibu Waziri Nderiananga

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mhe. Ummy Nderiananga amesema Serikali inahitaji taasisi zake kuongeza ufanisi na tija katika utendaji wake ili kuongeza kasi ya maendeleo katika kukuza uchumi wa watanzania na Taifa kwa ujumla.

Ameyasema hayo wakati wa uzinduzi wa Bodi ya saba ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) Jijini Dar es Salaam na kuitaka bodi hiyo kuwa wabunifu huku wakifanya kazi kwa uadilifu na weledi ili kuchochea ushiriki wa wananchi katika shughuli za kiuchumi nchini.

"Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais shupavu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imewaamini hivyo ni jukumu lenu sasa kuonesha mchango wenu ikiwa ni pamoja na kusimamia utendaji wa Baraza. Naamini kwa umoja wenu na ushirikiano na Menejimenti ya (NEEC)

mtaweza kufanikisha hili na kuleta matokeo chanya katika kukuza uchumi wa Taifa,"Alisema Mhe. Ummy.

Mhe. Ummy amelikumbusha kwamba Mafanikio ya (NEEC) yanategemea kwa kiasi kikubwa miongozo na utendaji wa Bodi kuibua na kubuni mbinu zitakazoweza kuongeza wigo wa utoaji huduma za uwezeshaji kwa weledi na kufikia wananchi wengi.

"Bodi hii inatarajiwa kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha miaka mitatu, hivyo ni jukumu la Bodi kuhakikisha kuwa, Baraza linafikia malengo na matarajio ya wananchi katika kipindi chote cha utendaji wake,"Alisisitiza.

Aidha, aliielekeza Menejimenti ya (NEEC) kuhakikisha kuwa inapokea na kutekeleza maagizo na maelekezo yote yatakayotolewa na Bodi hiyo kwa lengo la kuboresha ufanisi katika kuimarisha utoaji huduma za uwezeshaji.

Awali akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu katika ofisi hiyo Bi. Stella Mwaiswaga alibainisha kuwa baraza hilo lina jukumu la kuhakikisha linasimamia utekelezaji wa sera ya Taifa ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi.

"Tunatambua umuhimu wa Baraza hili la Saba katika kuiongoza na kuisimamia (NEEC) kuhakikisha inafanya majukumu yake ipasavyo kwa ajili ya wananchi. Pia niwapongeze wajumbe wapya pamoja na wanaomaliza muda wao kwa kazi nzuri waliofanya katika baraza la sita,"Alibainisha Bi. Stella.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Bi. Beng'i Issa, aliahidi kwamba menejimenti ya (NEEC) kwa kushirikiana na wadau watafanya kazi kwa karibu na bodi hiyo ili kufikia azma ya Serikali ya kukuza ushiriki wa watanzania katika shughuli za kiuchumi yakiwemo makundi maalum wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu.



Naibu Waziri Ummy Nderiananga azindua zoezi la utafiti wa gharama za utapiamlo nchini

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Ummy Nderiananga amezindua Rasmi zoezi la utafiti wa gharama za Utapiamlo nchini, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maazimio ya viongozi wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kupitia mpango ujulikanao kama "The Cost of Hunger Study in Africa – COHA" ambapo Mheshimiwa DKt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameridhia ufanyike ikiwa ni nia yake ya dhati ya kuondoa utapiamlo nchini.

Uzinduzi huo Uliofanyika katika Ofisi wa Waziri Mkuu Jijini Dodoma Tarehe 14 Februari, 2024. Naibu Waziri Nderiananga Alisema, Lengo la utafiti ni kubainisha makadirio ya gharama zinazosababishwa na matatizo ya lishe duni yani utapiamlo kijamii na kiuchumi na hususan katika nyanja za sekta ya afya, elimu na nguvu kazi.

Aliongezea kuwa Tanzania itakuwa nchi ya 22 Barani Afrika kufanya utafiti kama huo pindi utakapokamilika na kwa mwaka 2024, takribani nchi 6 (ikiwemo Tanzania) zimeonesha utayari wa kufanya utafiti huo ili kuwezesha nchi kupanga malengo ya kupunguza upotevu wa pato ghafi itokanayo na utapiamlo na kuwekeza katika maeneo ya maendeleo.

Aidha, Naibu Waziri Nderiananga amewashukuru wataalamu wa Chakula na Lishe kwa kuishauri vyema Serikali juu ya umuhimu wa utafiti katika nchini

"Tunapokwenda kuandaa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050, niwashukuru wadau wetu wakiwemo Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto (UNICEF) ambao tayari wameshatoa fedha ambazo zitasaidia sana katika hatua muhimu za utafiti huu". Alisisita

Kwa upande wake Mwakilishi kutoka UNICEF Bw. John George ametoa pongezi kwa Serikali kwa kujiunga na Mpango wa COHA na kutambua nafasi ya mtoto ambaye ndiye mlengwa mkubwa katika mpango huo na kwa tafiti zilizotoa takwimu za utapiamlo nchini.

Akizungumza katika uzinduzi huo Mwakilishi Mkazi Nchini, wa Progamu ya Chakula Duniani (WFP) Bi Sarah Gibson Alisema Tafiti hizo zitasaidia kukabiliana na madhara yatokanayo na Utapiamlo nchini kama vile ukuaji kwa mtoto na huweza kuleta athari katika elimu ya mtoto na Maendeleo ya Taifa kwa Ujumla.



## Benki ya NMB kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu

Uongozi wa Benki ya NMB waahidi kuendelea kuunga mkono shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu katika kuhakikisha wanaimarisha mahusiano yaliyopo na kuendelea kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu yao ya kuratibu shughuli za Serikali.

Hayo yameelezwa na Mkuu wa Idara ya Huduma za Kibenki kwa Serikali na Ofisi ya Makao Makuu Ndogo ya NMB- Dodoma, Bi Vicky Bishubo wakati walipotembelea na kufanya mazungumzo na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Jim Yonazi pamoja na Naibu wake Bw. Anderson Mutatebwa ofisini kwake Jijini Dodoma.

Alisema kuwa, katika kutoa huduma za kibenki ambazo zinahusu ofisi ya Waziri Mkuu wataendelea kuyafikia makundi mbalimbali ikiwemo vijana kwa kutoa huduma za kibenki popote walipo na hii itasaidia kusukuma juhudi za Serikali katika huduma za kifedha.

"Tumeendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, na hii haitokuwa mwisho tunaahidi kuendelea kufanya hivyo katika kuunga mkono shughuli mnazotekeleza," alisema Vicky

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi alisema kuwa, Benki ya NMB imefanya jambo muhimu kuitembelea ofisi yake na kueleza namna ilivyojipanga kuhakikisha inaunga mkono shughuli za Serikali na kuwasihi waendelee kufanya hivyo kadiri inavyofaa.

"Ninawapongeza NMB kwa moyo huu na mmetupa kuona umuhimu wa kuimarisha umoja uliopo nitoe wito muendelee kutoa huduma bora za kibenki kwa jamii yetu ili wananchi waendelee kunufaika na uwepo wenu na kujiletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla," alisema Dkt. Yonazi

.

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na
kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.




2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz